Pambano Kuu

Utangulizi

“Jamii yote ya wanadamu sasa imo katika pambano kuu baina ya Kristo na Shetani kuhusu tabia ya Mungu, Sheria yake na Utawala wake juu ya ulimwengu wote. Mapigano haya yalianzia mbinguni wakati kiumbe aliyeumbwa na kutunukiwa uhuru wa kuchagua , kwa kujiinua akawa Shetani, mpinzani wa Mungu na akaongoza sehemu ya malaika katika maasi. Akapenyeza roho uasi katika ulimwengu huu alipowaongoza Adamu na Hawa kwenye dhambi. Dhambi hii ya kibinadamu ilikuwa na matokeo ya kupotosha sura ya Mungu katika wanadamu wote, uchafuzi kwa ulimwengu ulioumbwa na mwishowe uteketezwaji wakati wa gharika iliyoonea ulimwenguni pote. Ikitazamiwa na viumbe wote, dunia hii ikawa uwanja wa pambano la ulimwengu wote, na ambalo kutokana nalo haki ya Mungu wa upendo hatimaye itathibitishwa. Katika kuwasaidia watu wake katika pambano hili, Kristo anamtuma Roho Mtakatifu na malaika watiifu kuwaongoza kuwalinda na kuwategemeza katika njia ya wokovu.” (Ufu.12:4-9; Isa.14:12-14; Eze.28:12-18; Mwa.3; Rum.1:19-35; 5:12-21; 8:19-22; Mwa.6-8; 2Pet.3:6; 1Kor.4:9; Ebr.1:14)

Maandiko hudhirisha kuwapo pambano kali baina ya wema na uovu, baina ya Mungu na Shetani, pambano ambalo limejumuisha ulimwengu wote. Kujifunza jambo hili kutasaidia kujibu swali kwa nini Yesu alikuja duniani?

Kuhusishwa kwa Ulimwengu Wote

Siri ya siri, pambano baina ya wema na uovu liliianzia mbinguni. Inawezekanaje kwenye mbingu takatifu, kutokee uovu? Malaika, wenye hadhi kubwa kuliko wanadamu (Zab. 8:5) waliumbwa ili kuhusiana na Mungu (Uf. 1:1, 3:5, 5:11).

Wakiwa na nguvu nyingi na watii kwa amri za Mungu (Zab. 103:20) ni roho watumikao (Ebr.1:14). Kwa ujumla malaika huwa hawaonekani, mara kadha wa kadha hutokea na kuonekana kama wanadamu (Mw. 18, 19, Ebr. 13:2). Ilikuwa katika moja wa malaika hawa ndipo dhambi ilikoanzia.

Asili ya pambano

Ikimtumia mfalme wa Babeli na wa Tiro kama vielelezo vya Lusifa, Biblia hueleza jinsi pambano lilivyoanza. Lusifa alikuwa kerubi afunikaye (Isa14:12 Eze. 28:14). Maandiko yanasema moyo wake uliinuka kwa sababu ya uzuri, “ukaiharibu hekima kwa sababu ya mwangaza wako” (Eze. 28:17).

Lusifa alikataa kuridhika na hadhi aliyopewa. Akanuia kudai makuu (Isa. 14:12-14). Japo alitaka nafasi ya kuwa Mungu, alikataa tabia yake. Vituko vyake, vilipumbaza malaika, hadi baadhi yao, theluthi moja (Uf. 12:4) wakaungana naye, kumpinga Mungu.

Wanadamu waliingiaje kwenye pambano?

Baada ya kufukuzwa mbinguni (Uf. 12:10-13), aliwashawishi Adamu na Hawa wasimwamini Mungu (Mwa. 3:5). Hawa alipokula tunda walilokatazwa, alikuwa zana muhimu kumwangusha mumewe. (Mw. 3:6) Kwa kuwadanganya wazazi wetu, Shetani alichukua madaraka ya kuwa mtawala wa dunia. Shetani alimpa Mungu changamoto kutoka kwenye makao makuu yake mapya, duniani.

Athari kwa wanadamu

Athari za pambano baina ya Kristo na Shetani zilikuwa dhahiri kwa kuwa dhambi iliharibu taswira ya Mungu. Japo Mungu alitoa agano la rehema (Mwa. 3:15) mtoto wa kwanza wa Adamu alimwua mdogo wake (Mw. 4:8) Uovu uliendelea kuongezeka hadi Mungu akajawa huzuni na kuhitimisha "mawazo aliyonayo mwanadamu ni uovu tu moyoni mwake (Mwa. 6:5). Mungu alitumia gharika kusafisha dunia ya awali (Mwa. 7: 17 – 20). Kizazi kilichotokea baada ya gharika nao wakavunja agano na Mungu. Kwa kuwa Mungu aliamua hataingamiza dunia kwa gharika tena (Mwa. 9:1, 11), alichagua kuwachanganya lugha (Mwa. 11). Baadaye Mungu alimchangua Ibrahimu kwamba wanadamu wabarikiwe kupitia yeye (Mwa. 12: 1 – 3, 22:15-18). Uzao wa Ibrahimu nao hawakufuata agano, wakamwua Mkuu wa Agano, Yesu Kristo. (cf. Mdo.7:51-53)

Dunia, uwanja wa maonyesho kwa Ulimwengu Mzima. Kitabu cha Ayubu kinatoa maelezo wakati wawakilishi kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu walipokutana. Shetani alipoulizwa "umetoka wapi wewe", alijibu, anatokea duniani (Ayu. 1;6, 7, 2;7). Akaulizwa, umemwona Ayubu, ni mkamilifu (Ayu. 1:8). Shetania akajibu kwamba inalipa kuwa mwaminifu, si unamlinda, si umemtajirisha? Shetani akapewa ruhusa kumshambulia (Ayu. 1:9-2:7). Tumekuwa tamasha kwa wanadamu na malaika (1 Kor.4:9). Dhambi iliharibu mahusiano kati ya Mungu na wanadamu, na chochote kisichotokana na imani ni dhambi (Waru. 14:23). Kuvunja amri za Mungu ni matokeo ya kukosa imani kwa Mungu na kuharibu mahusiano na Mungu. Mungu anakusudia kurejesha mahusiano ya upendo, maana kwa upendo, tutaongozwa kumtii Mungu (Yoh. 14:15).

Kinachoshindaniwa : Ni nini hasa kinachotuhangaisha katika maisha na kifo?

Mamlaka ya Mungu na Sheria. Sheria ya Mungu ni muhimu kwa ustawi wa ulimwengu. Yeyote anayekosea, ni mwasi (1Yoh. 3:4). Badala ya kukiri kukosesha ulimwengu, Shetani humsingizia Mungu kuhusiana na Sheria yake.

Kristo na suala la Utii. Kwa kuyakabili majaribu hata akawa Kuhani wetu Mkuu (Ebr. 2:17) Yesu alifunga siku 40. Shetani alimwomba abadili mawe kuwa mikate ili kuthibitisha kwamba ni Mwana wa Mungu. (Mt. 4:3). Hapa Shetani alikuwa akikana tangazo la Mungu kwamba Yesu ni mwana mpendwa anayempendeza (Mt. 3:17). Shetani aliendelea kumjaribu kwa kutaka asujudiwe ili amgawie Yesu madaraka (Mt. 4:9). Ndipo Yesu alimwamuru aende zake, kwa kuwa ibada inamstahili Mungu pekee. (Mt.4:10).

Kalvari. Shindano lilidhihirika vema Kalvari. Shetani alikazana kufutilia mbali utume wa Yesu. Aliwatumia viongozi wa kidini kukomesha huduma ya hadhara ya Yesu (Yoh. 11: 45 – 54). Kwa kusalitiwa na mwanafunzi wake moja, Yesu alikamatwa, akashtakiwa na kuhukumiwa kifo (Mt. 26:63, 64, Yoh. 19:7). Kwa utii mkamilifu kwa Baba yake, Yesu alibaki mwaminifu hadi kifo. Mafao ya maisha na kifo cha Yesu yanavuka hata kwa wasio wanadamu. Akizungumzia msalaba, anasema hukumu ipo na mkuu wa ulimwengu huu atatupwa nje (Yoh. 12:31). Pia, kwa sababu ya hukumu kwa kuwa yule mkuu wa ulimwengu huu amekwisha hukumiwa (Yoh. 16:11). Upendo wa Yesu ulidhihirisha ukatili wa Shetani, na kuhakikisha anguko lake.

***Shindano kwa Ukweli ulio kwa Yesu*.** Leo shindano haliko tu kwenye mamlaka ya Kristo bali hata katika Neno lake. Biblia huhesabika kama kitabu cha kizamani wala siyo ufunuo wa Mungu. Wanatheolojia huhoji nafsi ya Yesu, kuzaliwa kwake na bikira, miujiza na ufufuo huwekwa kwenye mijadala.

Swali la Msingi. Yesu ni nani? (Mt. 16: 13, 14), Ndipo Yesu alipouliza, na ninyi mnaniona ni nani? Simoni Petro alijibu "wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye Hai. Yesu akasema, "Heri yako, Simon bar Yona kwa kuwa damu na nyama havikukufunulia wewe jambo hili, bali Baba yangu aliye mbinguni. (Mt. 16: 15 – 17). Leo kila moja wetu anakabiliwa na swali hilo.

Msingi wa mafundisho ya Biblia
Maandiko yanatualika kuutambua ukweli kama ulivyokatika Kristo (Efe. 4:21), kwa kuwa ndiye Kweli (Yoh. 14:6). Shetani anataka wanadamu watambue ukweli bila Yesu. Hivyo anaelekeza wanadamu ama kwa (1) Mtu/watu (2) ulimwengu wa asili unaoonekana (3) Maandiko (4) Kanisa. Wakati hayo yana nafasi kwa ajili ya kufunua ukweli, bado ni Yesu ndiye aliyeviumba vyote. Kuitenga Biblia na Yesu, ni kuiacha kweli, njia na uzima (Yoh. 14:6).

Umuhimu wa Fundisho la Pambano Kuu
Fundisho hufunua pambano kali katika ulimwengu. Kwa maana kushindana kwetu si juu ya damu na nyama bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu majeshi ya pepo wabaya, katika ulimwengu wa roho (Efe. 6:12).

Fundisho hutufanya tukae tukikesha. Kuelewa fundisho hutufanya tupambane. Ushindi wawezekana katika Kristo (Zab. 24;8). Paulo alishauri kuvaa silaha zote (Efe. 6:13 – 18). Ni fursa ya pekee kukaa tukisubiri kwa imani, tukimtegemea Yeye aliyetufanya zaidi ya washindi (Rum. 8:37)

Huelezea kwa nini tunateseka sasa. Aliyependa haki na kuchukia maasi (Ebr. 1:9) siye wa kulaumiwa kwa machungu yaliyoko duniani. Ni shetani ndiye wa kulaumiwa kwa ajali zote, vifo, machungu na huzuni.

Huelezea jinsi Yesu anavyojali. Roho Mtakatifu aliwekwa kukaa nasi hadi Yesu atakaporudi (Mt. 28:20, Yoh. 14;26) Malaika nao wamewekwa kusaidia wanadamu waokolewe (Ebr. 1:14) Ushindi wetu umehakikishwa.

Hufunua Msalaba ulivyo muhimu kwa ulimwengu wote (Uf. 12:11)